BAJUNI

# MUONGODHO WA MWALIMU
# KIVANGO 2


Yumna Hamid Titi

Fuad Aroi

Yumbe Athman



TWAWEZA COMMUNICATIONS
Working Towards a Better World

Shungwaya Welfare Association
Umoja ni Nguvu

SWAHILI RESOURCE CENTRE
Old Town, Sir Mbarak Hinawy Road
Mombasa

Kimechapishwa na:

Twaweza Communications Ltd.
Jumba la Twaweza, Barabara ya Muthithi
Mpesi Lane
S.L.P. 66872 - 00800 Nairobi, Kenya
Simu: +(254) 020 269 4409; 0727 427740
Barua pepe: info@twawezacommunications.org
Wavuti: www.twawezacommunications.org

©Haki a kunakili nḏa Twaweza Communications
Chapisho la Kwanḏa 2024

**ISBN: 978-9966-128-20-1**

Kiṯabu cha *Chusomeni Kibajuni* ni sehemu a nradi wa kulindra na kuimarisha uṯamaduni wa Vabajuni. Nradi huu huṯekeledhwa na kichuo cha Twaweza Communications, Shungwaya Welfare Association na Swahili Resource Centre. Undofadhiliwa na nfubasho wao wa British Council Protection Fund kwa ushirikiano na UK's Department for Culture, Media and Sport.

BRITISH COUNCIL
In partnership with
Department for Culture, Media & Sport
Cultural Protection Fund

Approved by KICD

# Aliomo

1: Sukuli . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 1

2: Sukuli . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 8

3: Vaṉama Va Kuewa . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 14

4: Usafi . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 19

5: Usalama . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 25

Approved by KICD

# SHUKURANI

Dhiṯabu dha *Chusomeni Kibajuni* ni sehemu a juhudi a kulindra na kuimarisha uṯamaduni wa Vabajuni. Chwaṯoa shukurani kwa mfuko wa British Council Protection Fund kwa nsaada ulochuwedhesha kuanḏika na kuchapisha dhiṯabu hidhi. Bila nsaada wavo ingalikuva tabu sana kuvapa vana va Kibajuni nafasi a kuifundrisha kusoma na kuanḏika Kibajuni. Chwavashukuru Dkt. Rukiya Harith na Nafisa Awadh kwa ushirikiano wavo na vaanḏishi kachika haṯua dhoṯe dha kuanḏika nfulululidho wa *Chusomeni Kibajuni*. Vaandishi va dhiṯabu hidhi – Yumna, Aroi na Yumbe – valiiṯolea kushiriki na kumalidha kuanḏika. Chwavashukuru sana kwa nchango huu muhimu. Pia chwanshukuru Athman Tora (Lalavani) na vale voṯe chufanyao navo kadhi hii adwimu a kuhifadhi na kuimarisha uṯamaduni wa Vabajuni.

Kimani Njogu,  Twaweza Communications
Omar Lali, Shungwaya Welfare Association
Athman Lali Omar, Swahili Resource Centre

Juni, 2024

# 1 SUKULI

## ISOMO LA KWANḎA

### MAḎA KURU: KUSIKIDHA

**MAḎA NDRODI: KUANḎAMA MAAGIDHO**

**Maṯokeo maalumu aṯarajiwao:**

Kusikilia mwisho wa kipindri, mwanafunḏi awedhe:

a) Kusikidha maagidho

b) Kusikidha maagidho kwa udhuri

**Maregeleo:** Kiṯabu cha mwanafunḏi ubasho wa 1

**Dhifaa dha kufundrishia:** Chachi, kifaa cha kidigichali.

**Suali ḏaḏisi**: Kwa nini chuanḏame maagidho?

**Uṯaraṯibu wa kufundrishia:**

- Changulidha kipindri kwa kuvavulidha vanafunḏi vachaye shuhuli dhifanyikadho sukuli.
- Angika chachi ubavoni na uvavulidhe vachambue ni nini vavonacho.
- Vambie vafungue dhiṯabu dhavo ubasho wa1, na vasikidhe maagidho a mwalimu.
- Mwalimu avaongodhe vanafunḏi kuangalia picha kweṉe kifaa cha kidigichali na avaagidhe vaanḏame maagidho kulingana na picha vavonadho.
- Mwalimu adhingaṯie vanafunḏi veṉe mahiṯaji maalumu.

## ISOMO LA PILI

## MAḎA KURU: KUDHUNGUMUDHA

## MAḎA NDRODI: KUṮOA MAAGIDHO

**Maṯokeo maalumu aṯarajiwao:**

Kusikilia mwisho wa kipindri mwanafunḏi awedhe:

a) Kuṯoa maagidho.

b) Kuimba wimbo kwa udhuri.

c) Kufurahia kuimba wimbo.

**Maregeleo:** Kiṯabu cha mwanafunḏi ubasho wa 2

**Dhifaa dha kufundrishia:** Dhifaa halisi km. kamba

**Suali ḏaḏisi**: Ni shuhuli gani dhifanyikadho darasani?

**Uṯaraṯibu wa kufundrishia:**

- Changulidha kipindri kwa kuvaambia vanafunḏi vachaye shuhuli dhifanyikadho darasani.
- Mwalimu avaagidhe vanafunḏi vaṯoke inḏe a darasa na aṯoe maagidho ili vaanḏame.
- Vakiva kweṉe dhikundri vanafunḏi vauke kamba.
- Mwalimu avashirikishe vanafunḏi vaimbe wimbo kweṉe ubasho wa 2.
- Vanafunḏi vaimbe wimbo kwa sauṯi huku vakiuka kamba.
- Kachika makundri, mwalimu avaagidhe vanafunḏi vaṯabe shuhuli mbalimbali dha darasani.
- Mwalimu adhingaṯie vanafunḏi veṉe mahiṯaji maalumu.

## ISOMO LA CHACHU

## MAḎA KURU: KUSOMA

### MAḎA NDRODI: KUSOMA MICHORO

**Maṯokeo maalumu aṯarajiwao:**

Kusikilia mwisho wa kipindri, mwanafunḏi awedhe:

a) Kuchambua michoro ipachikanao kachika madhingira a sukuli.

b) Kuchunga senchensi kwa kuchumia michoro.

**Maregeleo:** Kiṯabu cha vanafunḏi ubasho wa 3.

**Dhifaa dha kufundrishia:** Kadi maneno, Chachi eṉe senchensi.

**Suali ḏaḏisi:** Sukuli hufanywa shuhuli gani?

**Uṯaraṯibu wa kufundrishia:**

- Changulidha isomo kwa kuvavulidha vanafunḏi shuhuli vafanyadho darasani.
- Mwalimu aṯoe kadi maneno, vanafunḏi vadhisome.
- Vaagidhe vafungue dhiṯabu ubasho wa 3 ili vaenge michoro na vaeledhe vavonacho.
- Mwalimu achunge senchensi akichumia michoro.
- Vaagidhe vanafunḏi vachunge senchensi vakichumia michoro ilioko kweṉe kiṯabu ubasho wa 3.
- Hiṯimisha isomo kwa kuvashirikisha vanafunḏi vasome senchensi kweṉe chachi.
- Mwalimu adhingaṯie vanafunḏi veṉe mahiṯaji maalumu.

## ISOMO LA IṈE

## MAḎA KURU: KUSOMA

## MAḎA NDRODI: KUSOMA KIFUNGU

**Maṯokeo maalumu aṯarajiwao:**

Kusikilia mwisho wa kipindri, mwanafunḏi awedhe.

a) Kuṯabiri kifungu cha hadisi kwa udhuri.

b) Kusoma kifungu cha hadisi.

c) Kujibu masuali a kifungu cha hadisi.

d) Kufurahia kusoma.

**Maregeleo**: Kiṯabu cha mwanafunḏi ubasho wa 4

**Dhifaa dha kufundrishia:** Dhifaa halisi dha darasani.

**Suali ḏaḏisi:** Dhichu gani hupachikana darasani?

**Uṯaraṯibu wa kufundrishia:**

- Changulidha isomo kwa kuvavulidha vanafunḏi vachaye dhichu dhipachikanadho darasani.
- Vavoneshe dhifaa halisi darasani kama ubavo, ibavo la kuketia, choki nk.
- Vaekedhe vanafunḏi ubasho wa 4 ili vajaḏili michoro iliyoko kiṯabuni.
- Mwalimu asome kifungu kwa sauṯi na avape muḏa vanafunḏi vasome kimwa kimwa.
- Avaagidhe vanafunḏi vasome kifungu kwa sauṯi na aṯaue mwanafunḏi mmoya mmoya asome kwa sauṯi.
- Vape muḏa wa kujibu masuali a kifungu kachika dhiṯabu dhavo.
- Hiṯimisha isomo kwa kuvapa vanafunḏi nafasi a kuṯoa ufupisho kuhusu kifungu valichokisoma.
- Mwalimu adhingaṯie vanafunḏi veṉe mahiṯaji maalumu.

**Majibu alopendekedhwa:**

i. Sukuli a Kaa Chonjo.

ii. Bakora.

3 a) Hana bidii/ ndhivu.

b) Hungia sukuli kuchelewa.

iv. La!

v. Halisikii dawa.

vi. Kuva na bidii.

## ISOMO LA ṮANU

## MAḎA KURU: KUANḎIKA

### MAḎA NDRODI: KUANḎIKA MAINA A DHICHU DHA SUKULI

**Maṯokeo maalumu aṯarajiwao:**

Kusikilia mwisho wa kipindri, mwanafunḏi awedhe:

a) Kuchambua maina a dhichu dhipaṯikanadho sukuli.

b) Kuanḏika maina a dhichu kweṉe michoro.

c) Kuchunga senchensi kuchumia nchoro.

**Maregeleo:** Kiṯabu cha mwanafunḏi ubasho wa 6

**Dhifaa dha kufundrishia:** kadi maneno.

**Suali ḏaḏisi:** Ni dhichu gani hupachikana sukuli?

**Uṯaraṯibu wa kufundrishia:**

- Changulidha isomo kwa kuvavonesha dhichu darasani kama kichi, kiṯongoo, medha na uvambie vadhichambue.
- Vashirikishe kuchunga senchensi vakichumia maina a dhichu hidho.

- Vambie vafungue kiṯabu cha mwanafunḏi ubasho wa 6. Vakiva vavili vavili vachambue na kujadili picha dhilidhoko kiṯabuni.
- Vanafunḏi vaeledhanye dhichu hidho na vachaye maina.
- Vashirikishe kuchunga senchensi vakichumia maina hao.
- Mwalimu adhingaṯie vanafunḏi veṉe mahiṯaji maalumu.

## ISOMO LA SIṮA

## MAḎA KURU: KUANḎIKA

### MAḎA NDRODI: HARUFU KURU NA NDRODI

**Maṯokeo maalumu aṯarajiwao:**

Kusikilia mwisho wa kipindri, mwanafunḏi awedhe:

a) Kuanḏika senchesi kwa harufu kuru na ndrodi.

b) Kufurahia kuanḏika.

**Maregeleo:** Kiṯabu cha mwanafunḏi ubasho wa 7.

**Dhifaa dha kufundrishia:** kadi maneno.

**Suali ḏaḏisi:** Ni maneno gani ladhima aandwe kwa harufu kuru?

**Uṯaraṯibu wa kufundrishia:**

- Changulidha kipindri kwa kuvaagidha vanafunḏi kusoma harufu a-z kwa sauṯi.
- Ṯoa mifano ubavoni iloandikwa kwa harufu ndrodi na kubadilisha `kwa harufu kuru.
- Vashirikishe vaanḏike senchensi ubavoni kwa harufu kuru na ndrodi.
- Ṯoa kadi maneno dha harufu kuru na ndrodi ili vanafunḏi vachambue na kudhisoma.
- Hiṯimisha isomo kwa kuvaagidha vanafunḏi vajibu masuali ubasho wa 7.
- Mwalimu adhingaṯie vanafunḏi veṉe mahiṯaji maalumu.

**Majibu alopenḏekedhwa**:

i. MWALIMU ALIANḎIKA UBAVONI.

ii. SUKULI ECHU INA UVANḎA NKURU.

iii. MWANAFUNḎI HODARI HUPAWA DHAWAḎI.

i. kalamu angu inḏopoṯea.

ii. mwalimu husomesha kwa udhuri.

iii. mabuku aliraruka.

# 2 SUKULI

## ISOMO LA KWANḎA

### MAḎA KURU: KUSIKIDHA

**MAḎA NDRODI: KUANḎAMA MAAGIDHO**

**Maṯokeo maalumu aṯarajiwao:**

Kusikilia mwisho wa kipindri mwanafunḏi awedhe:

a) Kueledha maagidho apawao.

b) Kuanḏama maagidho

**Suali ḏaḏisi**: Mwalimu huṯoa maagidho gani sukuli?

**Maregeleo**: Kiṯabu cha mwanafunḏi ubasho wa 8.

**Dhifaa dha kufundrishia**: Chachi, kadi dheṉe maagidho

**Uṯaraṯibu wa kufundrishia:**

- Mwalimu avaongodhe vanafunḏi kueledha kuhusu picha dhiṯabuni ubasho wa 8.
- Kachika makundri mwanafunḏi mmoya aeledhe vangine vasikidhe kwa makini.
- Vanafunḏi vasome maagidho kachika kadi dha maneno na vaandame.
- Mwalimu avashirikishe kachika nṯedho wa kupichisha ujumbe kuṯoka kwa nchu mmoya hadi nngine kweṉe mashikio kwa siri.
- Vahimidhe umuhimu wa kuva makini vapawapo ujumbe.
- Mwalimu adhingaṯie vanafunḏi veṉe mahiṯaji maalumu.

**ISOMO LA PILI**

## MAḎA KURU: KUDHUNGUMUDHA

## MAḎA NDRODI: DHICHANDRAWILI/DHICHONDROVI

**Maṯokeo maalumu aṯarajiwao:**

Kusikilia mwisho wa kipindri mwanafunḏi awedhe

a) Kuchega na kuchagua dhichandrawili.

b) Kufurahia kuchega na kuchagua dhichandrawili kachika madhungumudho avo.

**Masuali ḏaḏisi**: Dhichandrawili ni nini? Dhichandrawili hukusudia nini kachika masomo?

**Maregeleo:** Kiṯabu cha mwanafunḏi ubasho wa 9.

**Dhifaa dha kufundrishia**: Picha dheṉe kuṯoa majibu a dhichandrawili.

**Uṯaraṯibu wa kufundrishia:**

- Vaeledhee vanafunḏi umuhimu wa dhichandrawili. Kisha vaavanye kachika makundri.
- Vakiva kachika makundri vanafunḏi vakumbusane dhichandrawili vadhiyivadho.
- Vanafunḏi vachegeane dhichandrawili kwa kushindrana.
- Mwalimu avapongedhe vanafunḏi na avahimidhe kukusanya dhichandrawili dhaidi.
- Mwisho mwalimu avape dhichandrawili vajibu dhiṯabuni ubasho 9.
- Mwalimu adhingaṯie vanafunḏi veṉe mahiṯaji maalumu.

**Majibu alopenḏekedhwa**

i. Kiachu.

ii. Dhichakwi.

iii. Nocha angani.

iv. Kishogo.



Approved by KICD

v. Kufuli.

vi. Kamasi.

vii. Kobe/fududu.

viii. Nlango.

ix. Kope.

x. Ulimi na menyo.

## ISOMO LA CHACHU

## MAḎA KURU: KUSOMA

### MAḎA NDRODI: KUSOMA SENCHENSI

**Maṯokeo maalumu aṯarajiwao:**

Kusikilia mwisho wa kipindri mwanafunḏi awedhe:

a) Kusoma senchensi kwa kudhingaṯia silabi.

b) Kuanḏika senchensi kwa udhuri.

c) Kufurahia kusoma na kuanḏika senchensi.

**Suali ḏaḏisi**: Ni siku gani hupandrishwa bendera sukuli?

**Maregeleo:** Kiṯabu cha mwanafunḏi ubasho wa 9.

**Dhifaa dha kufundrishia**: kadi maneno, Chachi eṉe senchensi.

**Uṯaraṯibu wa kufundrishia:**

- Vashirikishe vanafunḏi kusoma kadi maneno kachika dhikundri.
- Vanafunḏi vaundre senchensi na kudhisoma.
- Mwalimu avaongodhe vanafunḏi kusoma senchensi validhodhiundra kuchumia kadi maneno.
- Vanafunḏi vasome kwa pamoya senchensi dhilidho kiṯabuni ubasho wa 9.
- Vanafunḏi vashindrane kusoma senchensi dhiṯabuni.
- Mwalimu adhingaṯie vanafunḏi veṉe mahiṯaji maalumu.

## ISOMO LA IṈE

## MAḎA KURU: KUSOMA

## MAḎA NDRODI: KUSOMA KIFUNGU

**Maṯokeo maalumu aṯarajiwao:**

Kusikilia mwisho wa kipindri mwanafunḏi awedhe:

a) Kuṯabiri kifungu kabla a kukisoma.

b) Kusoma kifungu kwa udhuri na kwa kasi.

c) Kujibu masuali a kifungu.

**Suali ḏaḏisi**: Ni vanafunḏi gani hudhawaḏiwa?

**Maregeleo**: Kiṯabu cha mwanafundi ubasho wa 10 – 11

**Dhifaa dha kufundrishia**: Chachi, picha kiṯabu cha mwanafunḏi ubasho wa 10.

**Uṯaraṯibu wa kufundrishia:**

- Vaongodhe vanafunḏi kudhungumudha kuhusu picha kachika kiṯabu cha mwanafunḏi ubasho wa 10.
- Vanafunḏi vasome kifungu kimwa kimwa kisha vasome kwa sauṯi.
- Mwalimu avakumbuse kuanḏama maaḏili madhuri a kusoma.
- Vanafunḏi vachambue maneno magumu.
- Vaeledhe maana a maneno hao.
- Mwalimu avape masuali vanafunḏi vajibu dhiṯabuni.
- Vahimidhe kusoma dhaiḏi ṉumbani.
- Mwalimu adhingaṯie vanafunḏi veṉe mahiṯaji maalumu.

**Majibu alopenḏekedhwa**

i. Shuhuli a siku a dhawaḏi.



Approved by KICD

ii. Valofanya udhuri kachika nṯihani.

iii. a) Dhawaḏi dha alopacha alama nḏuri.

b) Mwanafunḏi mweṉe aḏabu.

c) Mwanafunḏi nsafi.

iv. Kusikilia sukuli mapema.

v. Peche.

## ISOMO LA ṮANU

## MAḎA KURU: KUANḎIKA

### MAḎA NDRODI: KUANḎIKA SENCHENSI

**Maṯokeo maalumu aṯarajiwao:**

Kusikilia mwisho wa kipindri mwanafunḏi awedhe:

a) Kuchambua michoro.

b) Kuandika senchensi kuchumia michoro.

c) Kufurahia kuanḏika na kusoma senchensi.

**Suali ḏaḏisi**: Ni mambo gani afanywao sukuli?

**Maregeleo:** Kiṯabu cha mwanafunḏi ubasho wa 12.

**Dhifaa dha kufundrishia**: Chachi, kadi maneno.

**Uṯaraṯibu wa kufundrishia:**

Vaavanye vanafunḏi kachika makundri. Vanafunḏi vadhungumudhe vavonacho kweṉe picha dhiṯabuni ubasho wa 12

- Vanafunḏi vasome maneno kweṉe kadi vashikanishe kadi kuundra maneno.
- Vanafunḏi vachunge senchensi kisha vadhisome.
- Vanafunḏi vaandike kwa haṯi safi kuhusu kisa kiṯokanacho na michoro kiṯabuni ubasho wa 12.
- Mwalimu adhingaṯie vanafunḏi veṉe mahiṯaji maalumu.

## ISOMO LA SITA

## MADA KURU: KUANDIKA

### MADA NDRODI: KUANDIKA SENCHENSI

**Matokeo maalumu atarajiwao:**

Kusikilia mwisho wa kipindri mwanafundi awedhe:

a) Kuchunga senchensi kwa kupanga maneno sawa.

b) Kusoma senchensi.

c) Kufurahia kuandika senchensi kwa hati nduri.

**Suali dadisi:** Senchensi nduri huundrwaye?

**Maregeleo**: Kitabu cha mwanafundi, ubasho wa 12.

**Dhifaa dha kufundrishia:** Kadi maneno.

**Utaratibu wa kufundrishia:**

a) Vakumbuse vanafundi namuna a kuundra maneno kwa kuchumia harufu.

b) Kachika dhikundri vanafundi vachumie kadi dha maneno kupanga senchensi vadhisome.

c) Vanafundi vavonyeshe senchensi dhavo mbee a darasa.

d) Vaongodhe kufanya dhoedhi ubasho wa12.

e) Vanafundi vasome kwa sauti.

f) Mwalimu adhingatie vanafundi vene mahitaji maalumu.



Approved by KICD

# 3 VAṈAMA VA KUEWA

## ISOMO LA KWANḎA

**MAḎA KURU: KUSIKIDHA**

**MAḎA NDRODI: NGANU**

**Maṯokeo maalumu aṯarajiwao:**

Kusikilia mwisho wa kipindri mwanafunḏi awedhe:

a) Kuṯoa nganu aloisikidha kuṯoka kwa mwalimu wake ihusuo vaṉama va kuewa.

b) Kujibu masuali a nganu alioṯolewa na mwalimu wake.

c) Kuva na adhima a kuea vaṉama va kuewa.

**Suali ḏaḏisi**: Kwa nini chukaea vaṉama ṉumbani?

**Maregeleo:** Kiṯabu cha mwanafunḏi ubasho wa 13

**Dhifaa dha kufundrishia:** Dhifaa halisi, kadi dha picha au michoro na kifaa cha kidigichali.

**Uṯaraṯibu wa kufundrishia:**

- Kusikidha na kufahamu nganu ihusuo vaṉama va kuewa.
- Kuirudia nganu kwa kuvaṯowa uvanḏani.
- Kuudhungumudhia umuhimu wa vaṉama va kuewa.
- Kujibu masuali ahusianao na nganu.
- Mwalimu adhingaṯie vanafunḏi veṉe mahiṯaji maalumu.

## ISOMO LA PILI

### MAḎA: KUDHUNGUMUDHA

### MAḎA NDRODI: FAIDA A VAṈAMA

**Maṯokeo maalum aṯarajiwao:**

Kusikilia mwisho wa kipindri mwanafunḏi
awedhe:

a) Kuchaya faida a vaṉama va kuewa.

b) Kuchambua faida a vaṉama va kuewa.

c) Kufurahia vaṉama va kuewa.

**Suali ḏaḏisi:** Vaṉama va ṉumbani vana faida gani?

**Maregeleo:** Kiṯabu cha mwanafunḏi ubasho wa 14

**Dhifaa dha kufundrishia:** Kifaa cha kidigichali, Kadi maneno.

**Uṯaraṯibu wa kufundrishia:**

- Mwalimu avaongodhe vanafunḏi vasome kadi maneno dha vaṉama va kuewa.
- Kachika makundi vanafunḏi vachaye faida dha vaṉama va kuewa ṉumbani.
- Mwalimu avaongodhe vanafunḏi vadhiḏi kuchambua faida dha vaṉama va kuewa ṉumbani.
- Mwalimu adhingaṯie vanafunḏi veṉe mahiṯaji maalumu.

## ISOMO LA CHACHU

### MAḎA: KUSOMA

### MAḎA NDRODI: KUSOMA KWA SAUTI (NGANU)

**Maṯokeo maalumu aṯarajiwao:**

Kusikilia mwisho wa kipindri mwanafunḏi awedhe;

a) Kuchambua na kudhingaṯia alo muhimu kachika kifungu cha maanḏishi.

b) Kusoma senchensi pesi dhihusianadho na vaṉama va kuewa.

c) Kusoma kwa kupumbaa.

**Suali ḏaḏisi:** Vaṉama va ṉumbani vana umuhimu gani?

**Maregeleo:** Kiṯabu cha mwanafunḏi ubasho wa 15

**Dhifaa dha kufundrishia:** Dhifaa halisi, kadi dha picha au michoro.

**Uṯaraṯibu wa kufundrishia:**

- Kusoma senchensi kwa dhamu.
- Kuaiva maneno aganyao kachika kifungu cha maanḏishi.
- Kudhungumudhia ujumbe ulioko kachika kifungu cha maanḏishi.
- Kujibu masuali a kauli ahusuo kifungu cha maandishi.
- Mwalimu adhingaṯie vanafunḏi veṉe mahiṯaji maalumu.

**Majibu alopenḏekedhwa:**

1. Mwichuni.
2. Valikuva vakiliwa na simba.
3. Vaṯadhanya idhiva.
4. Vaṯakuva makwiji va midhigo.
5. Paka aṯashika paṉa.

## ISOMO LA IṈE

## MAḎA: KUANḎIKA

## MAḎA NDRODI: KUCHAYA HARUFU KACHIKA MAṈENO.

**Maṯokeo maalumu aṯarajiwao:**

Kusikilia mwisho wa kipindri mwanafunḏi awedhe:

a) Kuchambua na kudhichaya harufu dhilidhoko kachika maneno ahusianao na kiini cha maḏa.

b) Kuanḏika maneno mageni na asokuva mageni kwa kuchumia ufahamu wa sauṯi.

c) Kuusamini umuhimu wa harufu kachika kuanḏika.

**Suali ḏaḏisi:** Kwa nini ni muhimu kuṯamuka sauṯi dha harufu kachika maneno?

**Maregeleo:** Kiṯabu cha mwanafunḏi ubasho wa 16

**Dhifaa dha kufundrishia:** Dhifaa halisi, michoro, kadi dha maneno na kifaa cha kidigichali.

**Uṯaraṯibu wa kufundrishia:**

- Kupulika na kuchungudha maneno alioko kweṉe ishambu la maneno.
- Kudhichaya harufu dhalidhoundra maneno kweṉe ishambu la maneno.
- Kuanḏika maneno kwa udhuri.
- Kuṯamuka na kuanḏika maneno mageni kwa ushirikiano.
- Mwalimu adhingaṯie vanafunḏi veṉe mahiṯaji maalumu.

## ISOMO LA ṮANU

## MAḎA: KUANḎIKA

### MAḎA NDRODI: KUYADHA PENGO

**Maṯokeo maalumu aṯarajiwao:**

Kusikilia mwisho wa kipindri mwanafunḏi awedhe;

a) Kuyadha pengo kuchumia harufu.

b) Kusamini umuhimu wa kuanḏika kwa kuchumia harufu dhiṯakikanadho.

**Suali ḏaḏisi:** Uṯayadhaye pengo ili kuundra maneno?

**Maregeleo:** Kiṯabu cha Mwanafunḏi ubasho wa 17

**Dhifaa dha kufundrishia:** Michoro, kadi maneno na kifaa cha kidigichali.

**Ut̲arat̲ibu wa kufundrishia:**

- Mwalimu avaongodhe vanafund̲i kusoma kadi dha maneno.
- Vanafund̲i vabainishe maneno anaohusu van̲ama va kuewa.
- Mwalimu avaongodhe vanafund̲i kuchambua harufu dhilidhopungua kachika maneno.
- Vanafund̲i vaand̲ike maneno kwa ukamilifu.
- Mwalimu adhingat̲ie vanafund̲i ven̲e mahit̲aji maalumu.

**Majibu alopend̲ekedhwa:**

i. Ukandra

ii. Farasi

iii. Ng'ombe

iv. Hond̲oo

v. Mbudhi

vi. Kuku

vii. Ibit̲a

viii. Paka

ix. Imbwa

x. Ngamia

# 4 USAFI

## ISOMO LA KWANḒA

### MAḒA: KUSIKIDHA

**MAḒA: NDRODI: HADISI**

**Maṯokeo maalumu aṯarajiwao:**

Kusikilia mwisho wa kipindri mwanafunḏi awedhe;

a) Kusikidha hadisi kwa makini.

b) Kubaini dhichendro dha usafi dhilidhochaywa.

c) Kujibu masuali kuṯokana na hadisi.

**Suali ḏaḏisi:** Usafi una umuhimu gani?

**Maregeleo:** Kiṯabu cha mwanafunḏi ubasho wa 18

**Dhifaa dha kufundrishia:** Michoro, kifaa cha kidigichali

**Uṯaraṯibu wa kufundrishia:**

- Vaeledhe vanafunḏi umuhimu wa usafi.
- Mwalimu avasomee hadisi kiṯabuni avaongodhe vanafunḏi kusoma pia.
- Mwalimu avavulidhe masuali vanafunḏi vajibu kuṯoka kwa hadisi.
- Vaeledhe maana a maneno mapia.
- Vajibu masuali.
- Mwalimu adhingaṯie vanafunḏi veṉe mahiṯaji maalumu.

**Majibu alopenḏekedhwa**

i. Kusafi.

ii. Usafi wa madhingira.

iii. Kufanya usafi.Ṉumbani, sukuli na choni.

iv. Chufundrishane usafi.



Approved by KICD

## ISOMO LA PILI

## MAḎA: KUDHUNGUMUDHA

### MAḎA NDRODI: MADHUNGUMUDHO KUHUSU USAFI

**Maṯokeo maalumu aṯarajiwao:**

Kusikilia mwisho wa kipindri mwanafunḏi awedhe;

a) Kusoma madhungumudho kuhusu usafi.

b) Kujibu masuali.

c) Kufurahia madhungumudho kuhusu usafi.

d) **Maregeleo:** Kiṯabu cha mwanafunḏi ubasho wa 19

**Dhifaa dha kufundrishia:** Picha

**Uṯaraṯibu wa kufundrishia:**

- Mwalimu aṯauwe vanafunḏi vavili vaṯabe madhungumudho kachi a mwalimu na mwanafunḏi nchafu.
- Vashirikishe vanafunḏi vasome madhungumudho kiṯabuni ubasho wa 19 kachika dhikundri.
- Vanafunḏi vachaye shuhuli dha usafi wa nvili wa kila siku.
- Vanafunḏi vajibu masuali.
- Mwalimu adhingaṯie vanafunḏi veṉe mahiṯaji maalumu.

**Kadhi a dhiada:** vanafunḏi vafanye usafi ṉumbani.

**Majibu alopenḏekedhwa**

i. Kuhusu usafi.

ii. Radhia na Salama.

iii. Nchafu.

iv. Radhia.

v. Ndriyo, alinfundrisha Radhia kuhusu usafi.

## ISOMO LA CHACHU

## MAḎA: KUSOMA

### MAḎA NDRODI: SHAIRI

**Maṯokeo maalumu aṯarajiwao:**

Kusikilia mwisho wa kipindri mwanafunḏi awedhe;

a) Kubaini dhichendro dha usafi kachika shairi.

b) Kusoma na kukariri shairi.

c) Kufurahia kukariri shairi kwa mahadhi.

**Suali ḏaḏisi:** Usafi una umuhimu gani?

**Maregeleo:** Kiṯabu cha mwanafunḏi ubasho wa 20.

**Dhifaa dha kufundrishia:** Kifaa cha kidigichali.

**Uṯaraṯibu wa kufundrishia:**

- Mwalimu avasikidhishe vanafunḏi shairi kwa kuchumia kifaa cha kidigichali.
- Vanafunḏi valisome shairi dhiṯabuni kwavo.
- Vanafunḏi valikariri shairi kwa mahadhi.
- Mwalimu avaeledhee maana a maneno magumu.
- Vanafunḏi vafurahie shairi, valikariri na kuṯaba.
- Mwalimu adhingaṯie vanafunḏi veṉe mahiṯaji maalumu.



Approved by KICD

## ISOMO LA IṈE

## MAḎA: KUSOMA

### MAḎA NDRODI: SENCHENSI

**Maṯokeo maalumu aṯarajiwao:**

Kusikilia mwisho wa kipindri mwanafunḏi awedhe;

a) Kusoma senchensi kwa kuendreledha.

b) Kufurahia kusoma senchensi.

c) Kuva na hamu a kusoma.

**Suali ḏaḏisi:** Kuyiva kusoma kuna umuhimu gani?

**Maregeleo:** Kiṯabu cha mwanafunḏi ubasho wa 21.

**Dhifaa dha kufundrishia:** Kadi dha senchensi, kadi maneno.

**Uṯaraṯibu wa kufundrishia:**

- Vaveke vanafunḏi kweṉe dhikundri vasome kadi zeṉe maneno.
- Vanafunḏi vasaidiane kuchambua maneno kweṉe kadi.
- Vashirikishe kupanga kadi maneno kuchengedha senchensi.
- Vape kadi dheṉe senchensi vanafunḏi vasaidiane kudhisoma kwa sauṯi.
- Pamoya na vanafunḏi vasome senchensi kachika dhiṯabu dha vanafunḏi.
- Mwalimu adhingaṯie vanafunḏi veṉe mahiṯaji maalumu.

## ISOMO LA ṮANU

## MAḎA: KUANḎIKA

### MAḎA NDRODI: HAṮI NḎURI

**Maṯokeo maalumu aṯarajiwao:**

Kusikilia mwisho wa kipindri mwanafunḏi awedhe;

a) Kuanḏika kwa mpangilio bora na kwa haṯi nḏuri.

b) Kuanḏika kwa kudhingaṯia harufu dha mikia a iyu, kachi na a ṯini.

c) Kuṯamani kuva na mwanḏiko ndhuri.

**Masuali ḏaḏisi**: Kwa nini chuifundrishe haṯi?

**Maregeleo:** Kiṯabu cha mwanafunḏi ubasho wa 22.

**Dhifaa dha kufundrishia:** Kadi dheṉe senchensi (haṯi safi)

**Uṯaraṯibu wa kufundrishia:**

- Vakumbuse vanafunḏi kuhusu harufu, nfano dha kwendra iyu, dha kushuka ṯini na dha kubakia kachi.
- Vashirikishe kuanḏika kwa haṯi nḏuri ubavoni.
- Vanafunḏi vashiririkiane kuanḏika ubavoni kwa haṯi nḏuri.
- Vashirikishe kusoma senchensi hidho na kudhianḏika kitabuni.
- Mwalimu adhingaṯie vanafunḏi veṉe mahiṯaji maalumu.

## ISOMO LA SIṮA

## MAḎA: KUANḎIKA

## MAḎA NDRODI: KUUNGANISHA SILABI

**Maṯokeo maalumu aṯarajiwao:**

Kusikilia mwisho wa kipindri mwanafunḏi awedhe;

a) Kuunganisha silabi kuundra ineno.

b) Kusoma ineno.

**Maregeleo:** Kiṯabu cha mwanafunḏi ubasho wa 22.

**Suali ḏaḏisi:** Maneno huchengedhwaye?

**Dhifaa dha kufundrishia:** Kadi maneno/ harufu.

**Uṯaraṯibu wa kufundrishia:**

- Kachika dhikundri vape vanafunḏi kadi zeṉe silabi na harufu.
- Vaongodhe vanafunḏi vapange silabi vapache ineno.

- Vaongodhe vanafund̠i kuundra maneno kuchumia silabi alidhopawa, ubasho wa 22.
- Kachika dhikundri vanafund̠i vavoneshe maneno avo na vasome kwa saut̠i.
- Vanafund̠i vaand̠ike kit̠abuni.
- Mwalimu adhingat̠ie vanafund̠i ven̠e mahit̠aji maalumu.

**Majibu alopend̠ekedhwa:**

**A**

i. Maradhi.

ii. Choo.

iii. Madhingira.

iv. Kukusanywa.

v. Kipindrupindru.

**B**

i. sabuni.

ii. kukot̠a.

iii. mafucha.

iv. nsuaki.

v. kit̠ana.

# 5 USALAMA

## ISOMO LA KWANḎA

### MAḎA KURU: KUSIKIDHA

### MAḎA NDRODI: KUSIKIDHA MAAGIDHO

**Maṯokeo maalumu aṯarajiwao:**

Kusikilia mwisho wa kipindri, mwanafunḏi awedhe;

a) Kuanḏama maagidho kuhusu usalama wa ṉumbani.

b) Kuchaya ajali dhilidhoko kweṉe picha.

c) Kujadili mbinu dha kudhivia ajali.

**Maregeleo:** Kiṯabu cha mwanafunḏi ubasho wa 23.

**Dhifaa dha kufundrishia:** Dhifaa halisi (kisu, sinḏanu), kifaa cha kidigichali.

**Suali ḏaḏisi:** Uṯachumia mbinu gani kudhivia ajali?

**Uṯaraṯibu wa kufundrishia:**

- Changulidha kipindri kwa kuvavulidha vanafunḏi masuali kuhusu usalama.
- Vaagidhe vanafunḏi vafungue kiṯabu ubasho wa 23 na vasikidhe maagidho a mwalimu.
- Vashirikishe vanafunḏi vaenge picha na vanene vavonacho.
- Kachika dhikundri vanafunḏi vajadiliane mbinu dha kudhivia ajali.
- Hiṯimisha kwa kuchilia nkadho mbinu mbalimbali dha kudhivia ajali.
- Mwalimu adhingaṯie vanafunḏi veṉe mahiṯaji maalumu.

## ISOMO LA PILI

## MAḎA KURU: KUDHUNGUMUDHA

### MAḎA NDRODI: KUSIMULIA DHISA

**Maṯokeo maalumu aṯarajiwao:**

Kusikilia mwisho wa kipindri mwanafunḏi awedhe:

a) Kusimulia dhisa dha ajali kwa ufasaha.

b) Kuchaya kinga dha kuikinga na ajali.

c) Kufurahia kusikidha dhisa.

d) Kuva na mbinu dha kuikinga na ajali.

**Maregeleo:** Kiṯabu cha mwanafunḏi ubasho wa 24.

**Dhifaa dha kufundrishia:** Picha kiṯabuni.

**Suali ḏaḏisi:** Kwa nini wapenḏa kusimulia hadisi? Kwa nini wapenḏa kusikidha hadisi?

**Uṯaraṯibu wa kufundrishia:**

- Changulidha isomo kwa kudhungumudhia kuhusu usalama.
- Vavulidhe vanafunḏi vachaye mbinu dha kudhivia ajali.
- Vanafunḏi vafungue kiṯabu ubasho wa 24, vajadili picha.
- Vasimulie kisa kifupi kuhusu ajali.
- Vashirikishe vanafunḏi vasimulie dhisa vadhiivadho kuhusu ajali.
- Hiṯimisha isomo kwa kusisiṯidha asari dha ajali na vipi chuṯadhiepuka.
- Mwalimu adhingaṯie vanafunḏi veṉe mahiṯaji maalumu.

## ISOMO LA CHACHU

## MAḎA KURU: KUDHUNGUMUDHA

### MAḎA NDRODI: WIMBO

**Maṯokeo maalumu aṯarajiwao:**

Kusikilia mwisho wa kipindri, mwanafunḏi awedhe:

a) Kusoma shairi kuhusu usalama.

b) Kukariri shairi kuhusu usalama.

c) Kufurahia kukariri shairi kwa mahadhi.

**Maregeleo**: Kiṯabu cha mwanafunḏi, ubasho wa 25.

**Dhifaa dha kufundrishia:** Chachi

**Suali ḏaḏisi:** Wimbo husaidia vipi kuṯoa ujumbe?

**Uṯaraṯibu wa kufundrishia:**

- Changulidha isomo kwa kuvaeledha vanafunḏi umuhimu wa usalama.
- Angika chachi na uvaambie vanafunḏi vajadili kimakundri.
- Vaagidhe vanafunḏi vafungue kiṯabu ubasho wa 25 vasome wimbo kwa sauṯi.
- Mwalimu aeledhe ujumbe ulioko kweṉe wimbo hoo.
- Vashirikishe vanafunḏi vaimbe wimbo hoo kwa mahadhi.
- Mwalimu adhingaṯie vanafunḏi veṉe mahiṯaji maalumu.


Approved by KICD

## ISOMO LA IṈE

## MAḎA KURU: KUSOMA

## MAḎA NDRODI: HADISI

**Maṯokeo maalumu aṯarajiwao:**

Kusikilia mwisho wa kipindri mwanafunḏi awedhe:

a) Kusoma hadisi kuhusu usalama wa ṉumbani.

b) Kujibu masuali kwa ndomo kuṯoka kweṉe hadisi.

c) Kufurahia kusoma hadisi.

**Maregeleo**: Kiṯabu cha mwanafunḏi ubasho wa 26.

**Dhifaa dha kufundrishia:** Picha kiṯabuni.

**Masuali ḏaḏisi:** Muhusika kachika hadisi ni nyani? Hupachae ujumbe kachika hadisi?

**Uṯaraṯibu wa kufundrishia:**

- Changulidha kipindri kwa kuvavulidha vanafunḏi vaeledhe kisa chochoṯe ambacho vameshuhudia kuhusu ajali.
- Vambie vafungue kiṯabu cha mwanafunḏi ubasho wa 26, vakiva vavilivavili vaongodhe kuijaḏili picha iliyoko kiṯabuni.
- Vape muda wa kuisoma hadisi hio kwa makundri kisha uṯaue baadhi avo vasome kwa sauṯi darasani kila mmoya aya moya.
- Vape muḏa vajaḏili masuali a hadisi kisha kila mmoya aanḏike majibu kachika dhiṯabu dhavo.
- Mwalimu adhingaṯie vanafunḏi veṉe mahiṯaji maalumu.

## ISOMO LA ṮANU

### MAḎA KURU: KUANḎIKA

### MAḎA NDRODI: KUANḎIKA SENCHENSI

**Maṯokeo maalumu aṯarajiwao:**

Kusikilia mwisho wa kipindri mwanafunḏi awedhe:

a) Kuanḏika senchensi kuchumia nchoro.

b) Kusoma senchensi.

c) Kufurahia kuanḏika na kusoma senchensi.

**Maregeleo:** Kiṯabu cha mwanafunḏi ubasho wa 28.

**Dhifaa dha kufundrishia:** Chachi, kadi maneno.

**Masuali ḏaḏisi:** Michoro husaidia vipi? Usalama una umuhimu gani?

**Uṯaraṯibu wa kufundrishia:**

- Changulidha isomo kwa kueledhea umuhimu wa kudhingaṯia usalama.
- Vambie vafungue kiṯabu cha mwanafunḏi ubasho wa 28, vaongodhe kujaḏili picha kiṯabuni.
- Vavoneshe kadi dha maneno, vanafunḏi vadhisome kisha vaagidhe vachunge senchensi.
- Vape muda kujadili ṯena picha kiṯabuni na vachunge senchensi kuchumia michoro.
- Mwalimu adhingaṯie vanafunḏi veṉe mahiṯaji maalumu.

## ISOMO LA SIṮA

### MAḎA KURU: KUANḎIKA

### MAḎA NDRODI: KUPANGA SENCHENSI

**Maṯokeo maalumu aṯarajiwao:**

Kusikilia mwisho wa kipindri mwanafunḏi awedhe:

a) Kupanga senchensi kupacha kifungu sahihi.

b) Kusoma senchensi.

c) Kufurahia ubunifu wa kuanḏika senchensi.

**Maregeleo:** Kiṯabu cha mwanafunḏi ubasho wa 29.

**Dhifaa dha kufundrishia:** Chachi

**Suali ḏaḏisi:** Wadhingaṯia nini upangapo senchensi ili upache kifungu sahihi?

**Uṯaraṯibu wa kufundrishia:**

- Changulidha isomo kwa kuangika chachi ubavoni ilo na senchensi.
- Vaagidhe vanafunḏi vasome senchensi kwa sauṯi.
- Vaambie vafungue kiṯabu cha vanafunḏi ubasho wa 29, vaagidhe vasome senchensi.
- Vaeledhe vaṯakavopanga senchensi kwa ufasaha ili vapache kifungu sahihi.
- Hiṯimisha isomo kwa kuvashirikisha vanafunḏi vasome kifungu valichokipanga kwa sauṯi.
- Mwalimu adhingaṯie vanafunḏi veṉe mahiṯaji maalumu.